

**SHULE YA SEKONDARI AHMES**  
**KISWAHILI KIDATO CHA TATU**  
**KISWAHILI**  
**KAZI YA LIKIZO DISEMBA**

1. “Kiswahili ni kibantu” Jadili kauli kwa kutumia hoja tano za kiisimu na mifano ya kutosha.
2. Kwa sasa Kiswahili ni lugha iliyoenea sana ulimwenguni na kupata nguvu kimatumizi. Lakini kwa sasa Kiswahili kinakabiliwa na matatizo mengi sana. Jadili matatizo saba yanayokabili Kiswahili.
3. Eleza njia zilizotumika kueneza lugha ya Kiswahili Tanzania bara na visiwani kati ya karne ya 10 A.D na kabla yam waka 1800.
4. Kiswahili ni Kiarabu kwa jina lake lakini ni Kibantu kwa tabia yake. Tetea hoja hii kwa hoja nne na mifano ya kutosha.
5. Fafanua mchango wa mambo yafuatayo katika kukuza na kueneza Kiswahili nchini Tanzania wakati wa ukoloni.
  - a. Dini
  - b. Biashara
  - c. Utawala
  - d. Kampeni za kisiasa
6. “Fasihi simulizi hutumia vitu na wanyama katika fani yake lakini maudhui yake huhusu binadamu na maisha yake”. Jadili kauli hii kwa kutumia methali tano (5)
7. Kwa kutumia tamthiliya mbili mionganoni mwa zilizoorodheshwa, eleza jinsi waandishi walivyoonesha athari za utamaduni wa kigeni katika maadili ya jamii za kiafrika (hoja tatu kwa kila kitabu)
8. Chagua wahusika watatu wa kike kutoka katika kila tamthiliya kati ya ulizosoma kisha onesha kukubalika kwao kama kielelezo cha maisha.
9. “Si kila tungo ni sentensi”. Fafanua kauli hii kwa hoja zenye mifano ili kubainisha tofauti zake.
10. Changanua sentensi zifuatazo kwa njia ya matawi:
  - a) Katika nchi ya vipofu Chongo ni mfalme.
  - b) Wanafunzi walikunywa maji usiku kuccha.
  - c) Mwanafunzi aliyeleta vitabu hivi ameondoka.

11. (a) Nini maana ya ngeli za nomino?  
(b) kuna vigezo vingapi vya kuainisha ngeli za nomino katika Kiswahili. Fafanua faida na hasara za kila kigezo.
12. Kwa kutumia mifano ya rejesta nne eleza maana na matumizi ya rejesta za lugha.
13. Mkurugenzi mkuu wa shirika la reli ya Uhuru (TAZARA) S. L. P 2834 Dar es salaam ametoa tangazo katika gazeti la uhuru 6/12/2020 nafasi ya kazi za uhandisi na ukatibu muhtasi kwa wazalendo wenye elimu ya kiwango cha kidato cha nne. Andika barua kuomba kazi hiyo.
14. (a) Ni mambo yapi ya kuzingatia katika uandishi wa simu.  
(b) Andika mfano wa simu ya maandishi.  
Jifanye wewe ni meneja wa duka la vitabu Iringa Printers, andika tangazogazetini kuitangaza biashara yako.
15. Andika insha yenye maneno yasiyopungua 200 na yasiyozidi 300 kuhusu methali isemayo “samaki mkunje angali mbichi”.